بسم الله الرحمن الرحيم

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Sudan**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

**Jumapili, 01 Muharram 1446 H** **07/07/2024 M** **Na: HTS 1446 / 01**

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

# Kongamano la Cairo Larudisha tena Utawala ule ule Uliosababisha Migogoro na Kuichana Nchi

**(Imetafsiriwa)**

Jana, Jumamosi, tarehe 6 Julai 2024, lile linaloitwa Kongamano la Kisiasa na Majeshi ya Kiraia ya Sudan lilifanyika katika mji mkuu wa Misri, Cairo; nukta muhimu katika taarifa ya mwisho zilizotolewa zilikuwa: "...wanakongamano pia walisisitiza ulazima wa kushikamana na Azimio la Jeddah na kuzingatia taratibu za utekelezaji na maendeleo yake ili kuendana na maendeleo katika vita… Ama kuhusu njia ya kisiasa kutatua mgogoro huo, washiriki walikubaliana juu ya kuhifadhi Sudan kama nchi moja kwa misingi ya uraia, haki sawa, na serikali ya kiraia, kidemokrasia, kifederali…"

Kwa kuzingatia yale yaliyotajwa katika taarifa ya mwisho ya Kongamano la Cairo, sisi katika Hizb ut Tahrir/Wilayah ya Sudan tunathibitisha yafuatayo:

**Kwanza:** Wanasiasa walio mstari wa mbele katika matukio nchini Sudan bado wanafuata njia zao potofu za zamani, wanashangilia na kusherehekea masuluhisho ya mkoloni kafiri. Hawaoni suluhisho la machafuko ya Sudan, yaliyoundwa na mikono ya maadui, isipokuwa katika njama za maadui wenyewe, kwa hivyo methali isemayo, "Niponye kwa ugonjwa wenyewe!" inatumika kwao.

**Pili:** Kongamano hilo linarudisha utawala ule ule uliosababisha migogoro na kuichana nchi, hii ni kupitia kujadili serikali ya kiraia, kidemokrasia na ya kifederali. Ni serikali ile ile aliyoiunda kafiri mkoloni Muingereza nchini Sudan, kisha akawakabidhi wale aliowaundia kwa makusudi, hivyo wakafuata upotofu wake mpaka tukaifikia baada ya takriban miongo saba uhalisia huu mchungu.

**Tatu:** Wahudhuriaji wa kongamano hilo wamethibitisha kuwa wao ni sehemu ya sera ya Marekani ya kujaza ombwe hadi mapishi yake yenye sumu yatakapoiva na kuwapeleka Jeddah. Washiriki wa kongamano hilo hawana ruwaza ya kisiasa iliyo wazi zaidi ya kuregelea masuluhisho ambayo mkoloni kafiri Magharibi anawapatia kwa manufaa yao na dhidi ya maslahi ya watu wa Sudan.

**Nne:** Hatukuona katika kongamano hilo zaidi ya nyuso zinazohusishwa na mkoloni kafiri ambaye anamakinisha ukoloni na kutumikia miradi yake.

**Kwa kumalizia:** Tunawaambia watu wetu wa Sudan kwamba nyinyi ni Waislamu mnaomuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni Mola wenu Mlezi, Uislamu ni Dini yenu, na Muhammad (saw) kuwa ni Nabii na Mtume wenu, basi vipi mnakubali kuwa mtu anayehusishwa na maadui zenu makafiri, wasiokutakieni kheri, afanye kazi kutatua masuala yenu? Mwenyezi Mungu (swt) asema:

[مَّا يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَلَا الْمُشْرِكِينَ أَن يُنَزَّلَ عَلَيْكُم مِّنْ خَيْرٍ مِّن رَّبِّكُمْ]

**"Walio kufuru miongoni mwa watu wa Kitabu na washirikina hawapendi mteremshiwe kheri yoyote kutoka kwa Mola wenu Mlezi."** [Al-Baqara: 105].

**Mwisho:** Tunasisitiza kwamba hakuna suluhisho la migogoro ya Sudan na dunia nzima isipokuwa katika mfumo wa Uislamu na Shariah yake iliyonyooka inayotabikishwa na dola ya Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, ambayo wakati umewadia, Mwenyezi Mungu akipenda, na ambayo ni bishara njema ya kipenzi mteule (saw):

«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ. ثُمَّ سَكَتَ»

**"Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume, kisha akanyamaza."** [Imam Ahmad ameisimulia katika Musnad yake].

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Sudan**

**Simu:** 0912240143- 0912377707
**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com
**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.org
**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:**
www.hizb-ut-tahrir.info